Makundi ya Jamii yanaunga mkono Azimio la Tume ya Afrika la Kupinga Vita Vilivyoegemezwa kwa Mwelekeo wa Ngono na Utambulisho wa Jinsia

Muungano wa mashirika na watetezi wa haki za binadamu wanaofanya kazi kupanua haki za binadamu na za watu wanaunga mkono utekelezaji wa Azimio la *Ulinzi dhidi ya Vita na Ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya Watu kwa Misingi ya mwelekeo wao halisi au uliowekwa wa Ngono au Utambulisho wa Jinsia* na Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu katika kipindi cha 55 kilichofanywa Luanda, Angola, Aprili 2014.

Tunakumbuka utangulizi wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu ambapo mataifa yanachama yalizingatia sifa za tamaduni za kihistoria za Afrika na maadili ya ustaarabu wa Kiafrika na wakasema kwamba haya yanastahili kuwavutia na kuwekea tabia ya kutafakari mataifa yanachama kuhusu wazo la haki za binadamu na za watu. Tunaamini kwamba azimio limefanya uthibitisho na kuonyesha wazi wazi maadili haya.

Tunashukuru Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu, Shirika kuu lililopewa mamlaka katika Mkataba wa Afrika kwa kazi ya ulinzi na uhamasisho wa haki za binadamu Afrika, kwa uongozi wake na utambuaji wa kuwa na haki hizi kwa kila Mwafrika bila kuzingatia mwelekeo wao wa ngono, utambulisho wa jinsia au hali nyingine yoyote. Katika Mkataba wa Afrika, Tume ina jukumu la kuweka viwango vya haki za binadamu ambazo mataifa yote yanachama yanastahili kutii. Tume haipo ili kuzingatia chuki ya mataifa yanachama, ila ipo ili kuwajibisha mataifa wakati yanapokosa kutilia maanani viwango vya haki za binadamu. Azimio hili linatokea katika majira ambayo nchi nyingi zinatii au kuzingatia utekelezaji unaolenga watu wanaotazamiwa kuwa au tofauti na wasiowiana kwa mujibu wa jinsia, utambulisho wa jinsia na mwelekeo wa jinsia hivyo basi kuwa muhimu kwamba tume katika kushukuru hali ya masuala ya haki za binadamu yanayojitokeza katika bara, ilichagua kulenga ukiukwaji wa haki za binadamu ulioegemezwa kwa mwelekeo wa ngono na utambulisho wa jinsia.

Tunasherehekea Azimio ambalo kimasomaso huweka ukiukwaji wa haki za binadamu kwa msingi wa mwelekeo wa ngono na utambulisho wa jinsia chini ya wigo la Mkataba wa Afrika. Kufuatia miradi kama hiyo katika mifumo ya kikanda na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu ili kusuluhisha tatizo la kimataifa la ubaguzi wa jinsia moja na la chuki kwa waliobadilisha jinsia, Azimio hutoa msingi wa kisheria kwa wale wote wanaoteseka na kuishi chini ya tisho la vita kwa sababu ya mwelekeo wao wa kingono na utambulisho wa jinsia. Tunalichukulia azimio hili kama heshima kwa kumbukumbu za wale wote waliopoteza maisha yao katika vita kwa sababu walichukuliwa kuwa tofauti kwa misingi hii. Azimio hili ni hatua ya kwanza ya kuthibitisha usawa na heshima ya watu wote wa Afrika ambao walikuwa

wamelengwa na wanachukuliwa kama wananchi wa daraja la pili kwa sababu ya mwelekeo wao halisi au wa kuzingatiwa wa ngono na utambulisho wa jinsia.

Tunatoa mwito kwa wote waliojitolea na wanafanya kazi ili kuafikia kwa niaba ya wote Afrika haki ya uhuru kuhusu mili na maisha yetu na kwa heshima, bila ubaguzi na usawa kwa wote, kufanya kazi pamoja kwa bara ambalo ni huru na salama bila vita na kuhakikisha kwamba kiini cha Azimio kimetekelezwa na matafia yote yanachama.

Tunawatambua wanaharakati, watetezi wa haki za binadamu, makundi na taasisi ambazo zimefanya kazi bila kuchoka na kujitolea kwenye Tume ya Afrika, pamoja na wale waliounga mkono kazi hii kwa njia mbalimbali katika miaka minane iliyopita (chini kuna orodha ya makundi ambayo kati ya 2006 na 2014 yameshiriki katika sehemu fulani katika mchakato). Lengo letu pamoja la kuhakikisha kwamba Tume ya Afrika inatambua kuwa ukiukwaji wa haki za binadamu kwa msingi wa mwelekeo wa ngono na utambulisho wa jinsia zinahalalishwa chini ya Mkataba wa Afrika sasa linatambuliwa. Wakati kulipokuwa na shaka na kutamaushwa, tulisalia kuwa wima katika imani na kuamini kwamba Mkataba wa Afrika ni waraka wa kudumu unaotoa haki za binadamu na za watu kwa waafrika wote bila kuzingatia mwelekeo wa ngono, utambulisho wa jinsia. Tume sasa imethibitisha hili.

Mashirika ya Taifa Yasiyo ya Serikali: AIDS ACODEV; Aides Senegal; Alternatives-Cameroun;Arcad SIDA; Arc en Ciel Plus; Kituo cha Haki za Binadamu, Chuo Kikuu cha Pretoria; Mpango wa Wanawake Wanaojali; Mradi wa Watetezi wa Haki za Binadamu wa Magharibi na katika Pembe ya Afrika [EHAHRDP]; Muungano wa Heshima; Uhuru na Zurura Uganda; Jukwaa la Kustawisha Wanawake; Muungano wa Mashoga na Wasagaji Kenya; Jukwaa la Kuahamasisha Haki za Binadamu; Taasisi ya Haki za Binadamu ya Afrika Kusini; HOCA; Wavunjaji barafu Uganda; Mpango wa Kuendeleza Ubinadamu; Kituo cha Kimataifa cha Kuendeleza Haki za Afya; Lambda Msumbiji; LeGaBiBo; Matrix (Uswazi); Mouvement pour les Libertés Individuelles (MOLI); Haki Zangu; Tume ya Kitaifa ya haki za binadamu ya mashoga na wasagaji; PEMA-KENYA; Watu Wanaopinga Dhuluma ya Wanawake; Wasiotambuliwa Kingono Uganda; Mpango wa Haki Sawa;Mtandao wa Vijana wa Queer Africa; Muungano wa Queer ; Mwangaza wa Upinde Mshumaa; Muungano wa Utambulisho wa Upinde; SIPD; Stay Awake Network Activities; Spectrum Initiatives Uganda; Komesha Ukimwi; Pamoja kwa Haki za Wanawake; Haki za Afya na Usawa wa Wanawake;Mpango wa wanawake Wachanga; Shughuli za Kustawisha Vijana Zanzibar

Mashirika ya Kanda yasiyo ya Serikali: Wanaume wa Afrika wa Haki za Afya na Kingono; Muungano wa Haki na Ukimwi wa Afrika Kusini na Muungano wa Wasagaji Afrika; UHAI-EASHRI.

Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Serikali: Amnesty International, Heartland Alliance (GISHR) Wachunguzi wa Haki za Binadamu; Kituo cha Kimataifa cha Kulinda Haki za Binadamu (INTERIGHTS), Tume ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ya Mashoga na Wasagaji.

Kwa maswali zaidi wasiliana na -

1. Kene C. Esom, +2711 2426801, kene@amsher.net
2. Fadzai Muparutsa+2711 403 0004, fadzai@cal.org.za
3. Roselyn Odoyo +254 (020) 233 0050 / 812 7535roselyn@uhai-eashri.org

Imetolewa na: Wanaume wa Afrika wa Haki za Afya ya Ngono (AMSHeR), Muungano wa Wasagaji wa Afrika (CAL), Muungano wa Heartland (GISHR) na UHAI-EASHRI